Nambari ya Mtahiniwa ________________

SMZ

# BARAZA LA MITIHANI LA ZANZIBAR

## MTIHANI WA DARASA LA NNE

121 KISWAHILI

MUDA: SAA 2:00 Jumatano 21/11/2018, mchana

### MAAGIZO KWA WATAHINIWA

1. Mtihani huu una sehemu NNE (4) A, B, C na D.
2. Jibu maswali YOTE kutoka sehemu A na B. Swali MOJA (1) kutoka sehemu C na swali MOJA (1) kutoka sehemu D.
3. Andika nambari yako ya mtihani katika kila ukurasa.
4. Majibu yote yaandikwe katika nafasi zilizowekwa.

| KWA MATUMIZI YA WASAHIHISHAJI | | |
|---|---|---|
| NAMBARI YA SWALI | ALAMA | SAINI |
| 1. | | |
| 2. | | |
| 3. | | |
| 4. | | |
| 5. | | |
| 6. | | |
| 7. | | |
| 8. | | |
| 9. | | |
| 10. | | |
| JUMLA | | |

Mtihani huu una kurasa 14 zenye maandishi



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

Nambari ya Mtahiniwa _______________

## SEHEMU A: (Alama 20)

## UFAHAMU

Jibu maswali YOTE katika sehemu hii

Soma habari ifuatayo kisha jibu maswali yanayofuata.

Nchi yetu ya Tanzania ina wanyama wa aina nyingi. Baadhi ya wanyama hao ni kama vile chui, simba, swala, tembo, nyoka na twiga. Wanyama hawa wanahifadhiwa katika <u>mbuga</u> mbalimbali. Serikali yetu imewaajiri askari maalumu wa kuwalinda wanyama hawa ili kuhakikisha kuwa hawauwawi ovyo na <u>majangili</u>.

Wanyama wana faida nyingi. Miongoni mwa faida hizo ni kuwavutia <u>watalii</u> wanaokuja kuitembelea nchi yetu. Watalii huingiza fedha nyingi za kigeni. Pia wanyama ni mapambo ya nchi. Nchi isiyokuwa na wanyama haipendezi. Tunapowalinda wanyama hawa, watoto na <u>wajukuu</u> zetu watapata nafasi ya kuwaona.

Wanyama wana hasara pia. Endapo watatoroka kutoka kwenye mbuga wataweza kuharibu mimea na <u>kuwadhuru</u> watu. Mbali na hasara zilizopo lakini wanyama wana faida nyingi, hivyo hatunabudi kuwatunza vyema wanyama wetu.



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

Nambari ya Mtahiniwa ______________

1. Maswali

a) Taja wanyama wanne (4) wanaopatikana mbugani.

______________________________

______________________________

b) Kwa nini Serikali imewaajiri askari maalumu wa kuwalinda wanyama?

______________________________

______________________________

______________________________

c) Watalii huleta faida gani wanapokuja kuitembelea nchi yetu?

______________________________

______________________________

d) Bainisha hasara mbili (2) zinazoweza kusababishwa na wanyama.

i) ______________________________

______________________________

ii) ______________________________

______________________________



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

e) Andika faida mbili (2) za wanyama ambazo zimetajwa katika habari uliyoisoma.

i) ______________________________________________

______________________________________________

ii) ______________________________________________

______________________________________________

2. Lete maana ya maneno yafuatayo kwa mujibu wa habari uliyoisoma.

i. Mbuga

______________________________________________

ii. Majangili

______________________________________________

iii. Watalii

______________________________________________

iv. Wajukuu

______________________________________________

v. Kuwadhuru

______________________________________________



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

Nambari ya Mtahiniwa _______________

## SEHEMU B: (Alama 40)

## SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA

Jibu maswali YOTE katika sehemu hii

3. a) Eleza maana ya istilahi zifuatazo na utoe mfano mmoja (1) kwa kila istilahi.

   i. Nomino za kawaida

   ______________________________________________

   ______________________________________________

   ______________________________________________

   ii. Viwakilishi

   ______________________________________________

   ______________________________________________

   ______________________________________________

   iii. Kitenzi

   ______________________________________________

   ______________________________________________

   ______________________________________________



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

b) Tunga sentensi moja (1) kwa kila aina za vivumishi vifuatavyo, kisha pigia mstari vivumishi hivyo.

Kwa mfano:

Kivumishi cha kumiliki

Pesa zangu zimepotea.

i. Kivumishi cha sifa

______________________________________

ii. Kivumishi cha idadi

______________________________________

4. a) Badilisha sentensi zifuatazo ziwe katika wakati ujao.

i. Mgonjwa amelazimika kufanyiwa upasuaji.

______________________________________

ii. Babu anakwenda shamba.

______________________________________

iii. Jana tulifanya mtihani wa somo la Kiswahili.

______________________________________

b) Kanusha sentensi zifuatazo:

i. Watoto wamekunywa uji.

______________________________________



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

ii. Mkoba wangu una rangi nzuri.

_______________________________________________

5. a) Andika maneno yafuatayo kwa nambari.

i. Elfu nane, mia saba na hamsini na tano.

_______________________________________________

ii. Elfu kumi na mbili, mia mbili na ishirini.

_______________________________________________

iii. Laki tatu, elfu sabini na mbili na mia tisa.

_______________________________________________

b) Jaalia umemfanyia mwalimu wako makosa yafuatayo. Andika sentensi moja (1) ya kuomba msamaha kwa kila kosa.

i. Umechelewa kusafisha darasa.

_______________________________________________

_______________________________________________

ii. Hujamaliza kufanya kazi ya nyumbani uliyopewa.

_______________________________________________

_______________________________________________



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

6. a) Andika nambari zifuatazo kwa maneno.

i. 505

_______________________________________

_______________________________________

ii. 83,619

_______________________________________

_______________________________________

iii. 406,962

_______________________________________

_______________________________________

b) Andika sentensi zifuatazo kwa lugha ya Kiswahili.

i. I am very thirsty.

_______________________________________

_______________________________________

ii. Yesterday Zainab slept at quarter past ten.

_______________________________________

_______________________________________



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

Nambari ya Mtahiniwa _______________

## SEHEMU C: (Alama 20)

## FASIHI

### Jibu swali MOJA (1) tu katika sehemu hii

7. a) Andika beti tatu (3) za wimbo wowote uupendao.



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

b) Toa mafunzo mawili (2) yanayopatikana katika beti za wimbo ulizoziandika hapo juu.

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

8. a) Tegua vitendawili vifuatavyo:

i. Bendera ya Mwarabu inapepea.

_______________________________________________

ii. Babu kalala ndevu nje.

_______________________________________________

iii. Bibi hachoki kunibeba.

_______________________________________________

b) Eleza maana ya maneno yafuatayo na toa mfano mmoja kwa kila neno.

i. Nahau

_______________________________________________



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

ii. Misemo

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

## SEHEMU D: (Alama 20)

## UTUNGAJI

Jibu swali MOJA (1) tu katika sehemu hii

9. Andika barua ya kumuomba ruhusa mwalimu wako wa darasa kwa ajili ya kuhudhuria hitima ya jirani yako.

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

10. Taja vipengele vyote muhimu vinavyopaswa kuzingatiwa katika uandishi wa barua ya simu.



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

Nambari ya Mtahiniwa ________________

------------------------------



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org